



Umuhimu wa Uundaji wa Wahusika Mviringo katika Riwaya za Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Rosa Mistika

Gervas A. Kasiga

Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Article History

Received: 14.06.2026

Revised: 04.10.2026

Accepted: 12.10.2026

Published: 17.10.2026

Keywords

Fasihi

Kiswahili

Sanaa

Wahusika mviringo

How to cite:

Kasiga, G. A. (2026). Umuhimu wa Uundaji wa Wahusika Mviringo katika Riwaya za Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya Rosa Mistika. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 4(2), 27-39.

Copyright © 2026



Ikisiri

Makala hii inajadili umuhimu wa uundaji wa wahusika mviringo katika riwaya za Kiswahili. Riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) ya Euphrase Kezilahabi imetumika kuonesha namna wahusika mviringo wanavyowasilisha ujumbe kulingana na uhalisia wa mabadiliko ya mwanadamu. Mbinu za uchambuzi matini na mahojiano zilitumika katika ukusanyaji wa data. Nadharia ya Uhalisia imetumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji data, uchambuzi data, na matokeo yake. Matokeo yamebainisha kuwa uundwaji wa wahusika mviringo katika riwaya za Kiswahili una umuhimu katika kuonesha mabadiliko ya mwanadamu, kuimarisha uhalisia wa matukio ya riwaya, pamoja na kusaidia kuibua migogoro ya ndani na nje ya wahusika. Zaidi, ilibainika kuwa uviringo husaidia kuendeleza maudhui na kuongeza mvuto wa kisanaa wa riwaya. Kwa kuzingatia mjadala uliofanyika, makala imehitimisha kwa kauli kuwa, wahusika mviringo ni nyenzo muhimu ya kisanaa inayosaidia riwaya za Kiswahili kuwasilisha maisha ya binadamu kwa uhalisia pamoja na kuifanya kazi ya fasihi kuwa na mvuto wa kisaikolojia na kijamii.

Utangulizi

Riwaya ni mojawapo ya tanzu ya fasihi andishi inayotumia vipengele mbalimbali vya kifani na kimaudhui katika kuwasilisha masuala yanayoihusu jamii. Miongoni mwa vipengele muhimu vya kifani vinavyotumika katika ujenzi wa riwaya ni wahusika. Wahusika ni binadamu au viumbe wasio binadamu wanaotumiwa na mtunzi kuwasilisha yale anayoyakusudia kwa hadhira yake (Ponera & Kasiga, 2019). Muia, Mutua, na Makoti (2023) wanaeleza kuwa kipengele cha wahusika ni muhimu katika kazi ya fasihi kwa kuwa hushirikiana na vipengele vingine vya fani katika kufikisha ujumbe wa kazi husika. Kimsingi, wahusika hubeba matukio, migogoro, maudhui, na mitazamo mbalimbali inayowasilishwa na mwandishi. Uundaji wa wahusika hauishii katika kuwapa majina au kuwashirikisha katika matukio, bali huhusisha namna mwandishi anavyowapa sifa, historia, hisia, fikra, mienendo, saikolojia, haiba, na mahusiano yanayowafanya waonekane kama binadamu wenye maisha yanayoeleweka (Mlacha & Madumulla, 1995; Njogu & Chimerah, 1999; Ponera & Kasiga, 2019; Wamitila, 2024; Nyandwaro, 2024).

Fishelov (1990) anabainisha makundi mawili ya wahusika, ambao ni wahusika mviringo na wahusika bapa. Kifasihi, mhusika mviringo hutofautiana na mhusika bapa kwa kiwango cha uchangamano na mabadiliko anayoyapitia. Fishelov (ktj) anamwelezea mhusika mviringo kama mhusika mwenye haiba na tabia changamano. Mhusika huyu huwakilisha utu wa mwanadamu halisi akibeba pande mbalimbali za kitabia, kihisia, na kimawazo. Hali hiyo humfanya mhusika mviringo kuwa karibu zaidi na uhalisia wa mwanadamu kuliko mhusika mwenye tabia moja tu, yaani bapa.



Aidha, Fishelov (ktj) amebainisha sifa kuu nne za mhusika mviringo. Sifa hizo ni: Mosi, uchangamano; mhusika kuwa na tabia na hulka mbalimbali, si mwema au mwovu tu, bali anaweza kuwa na mazuri na mabaya kwa wakati mmoja. Pili, mabadiliko na maendeleo; ambapo mhusika mviringo hupitia mabadiliko makubwa ya kitabia, kimawazo au kihisia kadiri matukio ya hadithi yanavyoendelea. Uzoefu anaoupata mhusika huyu, huathiri maamuzi na matendo yake. Tatu, ni uhalisia unaomithilisha mwonekano na matukio yake na maisha halisi. Mwonekano unaoonesha hisia changamano, udhaifu na migogoro inayoweza kumpata mwanadamu. Nne, ni undani ambao huakisi historia, sababu za kutenda anachofanya, matamania, na migogoro ya ndani inayomsaidia msomaji kuelewa kwa nini mhusika anafanya maamuzi fulani. Kimsingi, sifa hizo zinachukua na misingi ya Nadharia ya Uhalisia inayobainisha kwamba wahusika wanapaswa kusawiriwa kiyakinifu ili kuakisi maisha ya kila siku katika jamii (Gouldin, 1961).

Rosa Mistika ni riwaya ya Euphrase Kezilahabi iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1971. Simulizi ya riwaya inamzungumzia Rosa Mistika kuanzia utotoni hadi mwisho wa maisha yake. Inaonesha mabadiliko mbalimbali anayopitia anapohama kutoka mazingira ya familia na kijiji kwenda shule na baadaye katika mazingira ya mjini na chuo. Rosa analelewa chini ya ulinzi mkali wa baba yake, Zakaria. Baadaye anaingia katika shule ya *Rozary* na hatimaye, Chuo cha Ualimu Morogoro ambako, anakutana na mazingira na changamoto mpya za maisha. Msururu huo wa mabadiliko unaifanya riwaya ya Rosa Mistika kuwa matini inayofaa kuchunguza umuhimu wa uundaji wa wahusika mviringo katika riwaya za Kiswahili.

Tafiti kadhaa zimejikita kuchunguza usawiri wa wahusika katika riwaya mbalimbali ikiwamo riwaya ya *Rosa Mistika*. Katika tafiti hizo, vipengele kama usawiri wa wanawake, makuzi ya wahusika, mitanziko, na mkengeuko wa malezi vimechunguzwa. Mathalani, Msigala (2024) anachunguza mkengeuko wa malezi katika riwaya ya *Rosa Mistika* na kubainisha matukio anuai yanayoakisi uhalisia wa jamii. Matukio hayo ni kama vile; ubakaji, kujiua, rushwa, umalaya, kupuuza ushauri, na matusi. Wakati Fuluge (2024), amechunguza mitanziko ya wahusika katika *Rosa Mistika* na *Kichwamaji*. Matokeo yake yamebainisha kuwa mitanziko inayowakabili wahusika hutokana na sababu za kijamii, kiutamaduni, na kifalsafa. Hivyo, kuwaathiri namna wahusika wanavyofikiri na kutenda.

Kwa upande wa Nkinde (2011) amechunguza motifu za safari na msako katika makuzi ya wahusika katika *Rosa Mistika* na Dunia Uwanja wa Fujo. Utafiti wake umehusisha namna hatua za makuzi na matatizo ya utotoni yanavyoweza kuwajenga wahusika. Anabaini kuwa baadhi ya matatizo wanayokumbana nayo huwa chachu ya mafanikio huku kwa wengine yakiwa kikwazo kinachochangia anguko. Mbali na hayo, tafiti za Muia, Mutua, na Makoti (2022) pamoja na Lyatuu (2011) zimebainisha usawirishaji kuwa wahusika wakuu katika *Rosa Mistika* wamewasilisha dhana mbalimbali za maisha katika ujenzi wa jamii bora.

Kimsingi, tafiti hizo zimesaidia kuonesha namna uhalisi unavyohitajika kwa kazi za kifasihi. Hata hivyo, zimeacha ombwe la kitafiti la kuchunguza umuhimu wa ujenzi wa wahusika mviringo katika riwaya za Kiswahili. Utafiti uliozaa makala hii, umemakinikia riwaya ya *Rosa Mistika* kwa kufafanua jinsi wahusika mviringo walivyo na umuhimu katika ujenzi wa kazi za kifasihi. Matokeo ya utafiti huu, yanaendeleza mjadala wa kitaaluma kuhusu ujenzi wa wahusika changamani katika riwaya za Kiswahili kwa muktadha wa kuakisi uhalisia wa kijamii.

Nadharia ya Uhalisia

Utafiti wa makala umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii iliasisiwa na Gustave Flaubert, ambaye anaeleza kuwa mtu hufikiria kwa kichwa na wala si kwa moyo wake (Gouldin, 1961). Nadharia ya Uhalisia ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika fasihi nchini Ufaransa mnamo



mwaka 1850 kwa lengo la kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kusawiri ulimwengu kama ulivyo. Miongoni mwa wanafasihi wa Kifaransa waliotumia nadharia hii ni Jules Husson Champfley. Mwandishi huyu aliwachora wahusika wake kulingana na mazingira halisi ya jamii (Gouldin, 1961). Kimsingi, nadharia hii shabaha yake kubwa ni kusawiri maisha ya binadamu na jamii kwa namna inayokaribiana na hali halisi. Uhalisi unajikita zaidi kumakinikia uzoefu, tabia, mahusiano, na mazingira ya kijamii (Kasiga, 2022).

Nadharia ya Uhalisia inaongozwa na misingi ambayo ni kusawiri maisha halisi ya jamii, kuwajenga wahusika kwa namna inayoaminika, kuhusisha wahusika na mazingira yao, kuonesha mabadiliko ya wahusika, pamoja na kuzingatia mahusiano ya mhusika na wahusika wengine. Misingi ambayo katika utafiti uliozaa makala hii imesaidia kumchunguza mhusika katika uhusiano na maisha ya jamii, mazingira na uzoefu anaoupitia badala ya kumtazama kama kiumbe aliyejitenga na jamii (Lukács, 1999).

Katika utafiti huu, misingi hii imetumika kama ifuatavyo: Msingi wa usawiri umetumika kuchunguza tabia, fikra, na matendo ya wahusika; msingi wa mabadiliko umetumika kufuatilia mabadiliko ya kitabia, kimawazo, kihisia au kimtazamo yanayothibitisha uviringo wao; msingi wa mazingira umetumika kubainisha namna mazingira na matukio yanavyochangia mabadiliko hayo; na msingi wa mahusiano umetumika kuonesha namna mwingiliano na migogoro na wahusika wengine unavyochangia katika ujenzi na mabadiliko ya wahusika. Hivyo, misingi hii imesaidia kubainisha namna wahusika wanavyojengwa, mabadiliko wanayopitia, na sababu zinazochangia katika mabadiliko hayo na, hivyo, kuthibitisha uviringo wao.

Methodolojia ya Utafiti

Makala hii, imetumia mkabala wa kitaamuli kwa kuwa inalenga kueleza na kufasiri namna mhusika mviringo alivyoumbwa na umuhimu wake katika riwaya. Usampulishaji lengwa umetumika ili kupata sampuli inayoendana na mada husika. Sampuli iliyotumika ni riwaya ya *Rosa Mistika*. Riwaya hii, iliteuliwa mahususi kwa sababu ina msuko wa matukio yanayojenga wahusika mviringo, ambao ni kiini cha mada iliyozaa utafiti wa makala. Kimsingi, katika utafiti huu riwaya tajwa imetumika kama kiwakilishi cha riwaya nyingine zinazoundwa na wahusika mviringo ndani yake.

Data zilipatikana kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Riwaya ya *Rosa Mistika* ilisomwa kwa kuzingatia matukio, matendo, kauli, mahusiano, mabadiliko ya tabia, na migogoro inayowahusu wahusika. Hatua hizo ziliwezesha kupatikana kwa wahusika mviringo wawili, yaani Rosa na Flora. Katika uchanganuzi, matukio ya wahusika hao yamechambuliwa kwa kuzingatia mpangilio wa maendeleo ya usimulizi wa riwaya ili kubaini mabadiliko yao kutoka hatua moja ya maisha kwenda nyingine. Uchambuzi huo, ulijikita katika vigezo vinne; ambavyo ni: Mabadiliko ya kimawazo, mabadiliko ya kitabia, mabadiliko ya kihisia, na namna mazingira pamoja na migogoro inavyochangia katika mabadiliko hayo. Mwisho, data zimewasilishwa kwa maelezo na kufasiriwa kwa kuhusianisha matukio ya matini na misingi ya Nadharia ya Uhalisia.

Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii, inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Imeundwa na sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina maelezo mafupi kuhusu wahusika mviringo waliobainishwa kutoka katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Katika sehemu ya pili, umetolewa ufafanuzi kuhusu umuhimu wa uundaji wa wahusika mviringo katika riwaya za Kiswahili.

Maelezo Mafupi Kuhusu Wahusika Mviringo

Kulingana na uchambuzi uliofanywa, mtafiti amebainisha wahusika mviringo wawili. Wahusika hao ni Rosa na Flora.



Rosa

Rosa Mistika ni mhusika mkuu katika riwaya hii. Mhusika ni kifungua mimba katika familia ya Bwana Zakaria na Bi. Regina. Familia hiyo imebarikiwa watoto sita, ambao ni: Rosa, Flora, Stella, Honorata, Sperantia, na Emanuel. Mwandishi amemwonesha Rosa kama msichana mrembo, mpambanaji (elimu na uhuru binafsi), na mhanga wa jamii. Katika suala la elimu, Rosa alikuwa msichana mwenye akili na anayependa masomo. Alijiunga na shule ya upili ya wasichana ya *Rosary* na kufaulu kwenda Chuo cha Ualimu cha Morogoro. Halikadhalika, Rosa ameonekana akijipambania uhuru wake. Mwandishi anaonesha jinsi baba yake alivyokuwa akimzuia kuongea na vijana wa kiume, anasema:

Rosa ... alianza kufikiri kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yupo Ukerewe mimi niko Usukumani. Baba anakaa akinichunga, anafikiri yeye atania? (Uk. 46).

Mbali na mazuo hayo, Rosa anaamua kufanya yale anayoyapenda. Mwishowe, anapata madhara makubwa ya kufukuzwa shule. Vilevile, katika hatua yake ya kimasomo anaonekana kubadilika kitabia na kutekwa na mihemko ya kimapenzi. Rosa anaonekana kulala na wanaume kemkem kuanzia sekondari hadi chuo.

Fauka ya hayo, Rosa amechorwa kama msichana mvumilivu. Mwandishi anamwonesha Rosa akivumilia mateso aliyotendewa na wanafunzi wenzake akiwa shule ya *Rosary*. Mathalani, anavumilia kutengwa na Deogratias, Bwana Thomas, na Charles ambao ni wanaume alioamini kuwa wangemwoa. Vilevile, hata baada ya kufukuzwa chuo, Rosa hakati tamaa anarudi kwa Mkuu wa Chuo ili kuomba nafasi ya kumaliza masomo yake. Kwa ujumla, mkusanyiko wa matukio anayoyapitia kama vile; kupata ulemavu wa sikio pamoja na kufanya ngono na wanaume wengi kunakomfanya aachwe na Charles (mchumba wake)—yanasababisha aamue kujiua.

Flora

Huyu ni mhusika msaidizi katika riwaya hii. Flora ni mdogo wake na Rosa. Ni mzaliwa wa pili katika familia ya Bwana Zakaria na Bi. Regina. Mwandishi anamchora Flora kama msichana anayejipenda na kujali mwonekano wake. Kama ilivyo kwa dada yake Rosa, mhusika huyu amekuzwa katika malezi makali ya baba yake. Malezi hayo badala ya kumjenga, yanakuwa kichocheo cha mabadiliko yake baada ya kuwa mbali na wazazi. Anapata mpenzi na kuishi naye akiwa bado yupo shule. Flora naye, anaoneshwa akijihusisha na wanaume zaidi ya mmoja.

Hata hivyo, mwandishi amemchora mhusika huyu kama mtu mwenye huruma na mlezi. Jambo hili linabainika baada ya kifo cha wazazi wake pamoja na dada yake, Rosa. Flora anabeba jukumu la kuwalea wadogo zake, huku akijiendeleza kielimu. Mwandishi anasema:

Flora aliwaomba masista waliokuwa wakikaa Kigunguli wamsaidie kutunza dada zake kwa muda wa miaka miwili. Hawakukataa, walimwonea huruma (uk. 150).

Kwa ujumla, wahusika hawa ndio waliotumika kama wahusika mviringo katika utafiti uliozaa makala hii. Wahusika hawa wamedhihirisha tija inayopatikana kwa wasomaji kupitia uchangamani wa wahusika mviringo katika kufikisha ujumbe wa kifasihi unaoakisi maisha halisi ya mwanadamu.

Umuhimu wa Uundaji wa Wahusika Mviringo katika Riwaya za Kiswahili

Matokeo ya utafiti uliozaa makala hii, yanaonesha kuwa wahusika mviringo wana nafasi muhimu katika kujenga na kuipa riwaya uhai wa kisanaa. Kupitia wahusika hao, mwandishi huweza kuonesha mabadiliko ya mwanadamu, kuimarisha uhalisia wa riwaya, kusaidia kuibua migogoro



ya ndani na nje, pamoja na kusaidia kuendeleza maudhui. Zaidi, riwaya zenye wahusika mviringo, huongeza mvuto wa kisanaa wa riwaya. Kwa msingi huo, sehemu inayofuata inawasilisha na kujadili umuhimu huo kwa kuzingatia uchambuzi uliofanyika kupitia riwaya ya *Rosa Mistika*.

Kuonesha Mabadiliko ya Mwanadamu

Uwapo wa wahusika mviringo katika riwaya hutokana na msuko wa matukio mbalimbali kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Jambo hili huonesha kwamba kiuhalisia mwanadamu hubadilika kutokana na uzoefu wa maisha tangu kuzaliwa hadi kufa kwake. Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, kila hatua inayopigwa na Rosa inachangia katika kumjenga upya. Anaanza akiwa katika mazingira ya kifamilia yanayodhibitiwa na baba yake, kisha anaingia katika mazingira ya shule, na baadaye anakutana na mazingira mapya ya kijamii na kimapenzi. Safari hii, inamfanya msomaji kumwona Rosa kama mhusika anayechukua maumbo mapya ya kimtazamo katika kukua kwake. Mabadiliko haya yana wajihi wa kibinadamu kwa kuwa na tabia changamani badala ya kubeba haiba moja iliyoganda.

Mathalani, katika mazingira ya kifamilia, mwandishi anamchora Rosa kama binti anayechungwa sana. Mfano, katika uk. 7 na uk. 11, tunamwona baba yake Rosa akimpiga kwa sababu alipokea barua kutoka kwa mwanaume. Mwandishi anaeleza:

Leta hiyo barua iko wapi? ...

Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikamtoka puani na mdomoni (uk. 7).

Hivyo ndivyo Rosa alivyolelewa; hivyo ndivyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa na baba yake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote (uk. 11).

Katika nukuu hii, tunaona safari ya Rosa kimakuzi na namna alivyokuwa akidhibitiwa na baba yake. Kutokana na malezi hayo, Rosa alimwogopa sana Zakaria na kuhofia kuwa na mpenzi wakati akiwa nyumbani na hata baada ya kwenda shule ya Upili. Rosa alibaki kuwa mwanafunzi mnyamavu na mwenye adabu mpaka pale alipohisiwa kuwa mlemavu kwa kutokujihusisha na mapenzi shuleni. Aidha, mwandishi anaendelea kuonesha mabadiliko ya Rosa kutoka katika familia kwenda shule na hadi kubadilika kitabia na kuangukia kwenye mapenzi ya kiholela. Ukurasa wa 46 - 47 mwandishi anasema:

Rosa alianza kufikiri kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yuko Ukerewe mimi nipo Usukumani. Baba anakaa akinichunga, anafikiri yeye atanioa? (uk. 46).

Rosa sasa alianza mapenzi. Alianza mapenzi lakini aliyaendea haraka sana kama mbwa aliyekata kamba. Aliona mvulana mmoja au wawili walikuwa hawamtoshi kwa urafiki. Mwaka huohuo aliwakubalia wavulana watano (uk. 47).

Kupitia nukuu hizi, tunaona jinsi mwandishi alivyomsuka mhusika huyu kwa kumpa unyumbulifu wenye kudhihirisha mabadiliko tangu utoto hadi utu uzima. Kimsingi, mabadiliko haya yanabainisha uviringo wa mhusika Rosa. Mwandishi angeweza kumchora Rosa kama mhusika mpole na mnyamavu kutokana na malezi ya Zakaria mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Hata hivyo, kutokana na umuhimu aliokuwa nao Rosa, mwandishi amemchora katika unyumbulifu ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa katika jamii. Mbali na Rosa, mwandishi anamchora Flora kama mhusika mviringo kwani tunaona mabadiliko yake kitabia ambayo yanachangiwa na mazingira aliyokuwa



nayo ukubwani. Katika riwaya hii, mwandishi anaeleza jinsi baba yao alivyojitahidi kuwachunga ili kuwaweka mbali na mikono ya wavulana. Mwandishi anasema:

Zakaria alijitahidi zaidi, katika kazi ya kuwachunga mabinti zake. Flora alikuwa sasa shule ya wasichana ya Mwanza ... alipokuwa anakuja likizo alikaripiwa kwa maneno ya kuogopesha na matusi (uk. 51).

Katika nukuu hii, tunaona jinsi ambavyo Flora alikuwa chini ya uangalizi mkubwa wa Zakaria ili asibadilike kitabia. Lakini mambo yalibadilika baada ya Flora kupelekwa shule na kuwa mbali na wazazi wake. Kiuhalisia, hii inaonesha kwamba ukali si kipimo cha mwisho cha kudhihirisha malezi bora kwa watoto. Mwandishi anasema:

Flora naye huko shule ya wasichana ... alikuwa ameshatoa mimba. “Mimba tu haiwezi kunifanya nikajiharibia maisha yangu kwa kuacha shule” (uk. 66).

Mabadiliko ya kitabia na kimawazo tunayoyapata katika nukuu hizi, yanatokana na jinsi ambavyo mwandishi amesuka matukio kwa lengo la kuonesha safari ya makuzi. Mambo haya yanasababisha kuundwa kwa wahusika mviringo wenye kubadilika kimawazo, kitabia, na kihisia.

Zaidi, mabadiliko haya yanachangiwa na kubadilika kwa mazingira waliyokuwa nayo wahusika, yaani kutoka Ukerewe kwenda Usukumani—Mwanza. Mazingira ambayo hawakuwa chini ya uangalizi wa mtu yeyote. Kwa ujumla, mambo haya yanajadiliwa na Nadharia ya Uhalisia, ambayo nayo inaamini katika mabadiliko. Nadharia hii, inamfafanua mhusika kama kiumbe asiyetulia. Katika msingi wa nne, mhusika anahusishwa na jamii na mazingira ili kupata uzoefu wa maisha halisi na kumtazama kama kiumbe asiyejitenga na jamii. Hivyo basi, kuundwa kwa wahusika mviringo husababisha riwaya ya Kiswahili kubeba mabadiliko ya kila siku ya mwanadamu.

Kuimarisha Uhalisia wa Riwaya

Uundaji wa wahusika mviringo humsaidia mwandishi kusawiri maisha halisi ya binadamu. Riwaya hujengwa na matukio, migogoro, mahusiano, na changamoto zinazoweza kutokea katika maisha halisi ya jamii. Mambo haya huifanya riwaya kutoonekana kama hadithi ya kubuni tu. Hii ni kwa sababu wahusika hawa hubadilika kimawazo, kihisia, kitabia, na kimtazamo kutokana na mazingira na matukio wanayopitia. Kwa hiyo, mabadiliko yao yanaifanya tabia ya binadamu katika riwaya isiwe ya upande mmoja au isiyobadilika. Huufanya uumbaji anaoufanya mwandishi umthilishe maisha halisi ambako mtu anaweza kufanya maamuzi tofauti kulingana na hali anazokabiliana nazo kila uchwao.

Ndani ya *Rosa Mistika*, mhusika Rosa amejengwa kwa namna bora ya kubainisha hoja hii. Hii ni kutokana na kuwa maisha yake yanatawaliwa na matukio anuai yenye uhalisia. Umviringo wa mhusika huyu unamwezesha mwandishi kuonesha kwamba maisha ni machaguo. Zaidi, unathibitisha kwamba maamuzi mengi ya mwanadamu huathiriwa na mazingira, mahusiano, na changamoto zinazomkabili. Katika simulizi ya riwaya hii, mabadiliko ya Rosa yanapowasilishwa kwa namna inayoakisi maisha halisi, yanampa mhusika wajihi wa kibinadamu na, hivyo, kumfanya Rosa asionekane kama mhusika wa kubuni tu. Hali hiyo humfanya msomaji amtazame mhusika huyu kama mtu halisi anayepitia matatizo yanayoweza kutokea katika maisha ya kila siku. Mathalani, katika riwaya hii, mwandishi ameonesha matukio kama utoaji mimba, mateso, na kifo. Anasema:

Rosa alitoa tena mimba alipoingia katika mwaka wake wa pili. Wengine walisema kwamba ilikuwa mimba ya tatu; wengine walisema kwamba ilikuwa mimba ya nne (uk. 66).



Katika nukuu hiyo, tunamwona mwandishi akimwelezea Rosa katika matukio ambayo yanaonesha uhalisia wa maisha ya vijana walioko vyaoni. Kama ambavyo imekuwa ikiripotiwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, ni dhahiri shayiri kwamba katika zama hizi wanachuo wamekuwa wakishuhudiwa kutoa mimba au wakati mwingine kutupa vichanga vyaoni. Kati ya sababu zinazowasukuma wafikie hatua hizo ni woga dhidi ya wazazi wao. Matukio haya aghalabu, husababisha vifo. Katika kulielezea jambo hili katika riwaya, mwandishi katika ukurasa wa 66 anaonesha mhusika Flora akitoa mimba mara kadhaa kwa kisingizio cha kutokutaka kujiharibia maisha yake ya baadaye kwa kuacha shule.

Pia, mwandishi ameonesha tukio la mateso kupitia mhusika Rosa. Tukio hili linabainisha uhalisia wa maisha ya shuleni. Rosa anateseka, anatengwa na wanafunzi wenzake kwa sababu alisema ukweli mbele ya walimu kuhusiana na wanafunzi waliokuwa na mahusiano na wanaume nje ya shule. Jambo hilo lilisababisha wanafunzi hao kufukuzwa shule huku likichochea fitina kuongezeka dhidi ya Rosa. Mwandishi anasema:

Alifunua deski lake kuchukua kitabu, hakuweza kuamini macho yake.
Alianza kulia kwa sauti. Daftari zake zote zilikuwa zimechanwa
vipandevipande lakini chuki haikuisha. Rosa alichukiwa sana. Alipojaribu
kukaa na kuongea na wenzie walimkimbia na kumwacha peke yake. Rosa
alikonda (uk. 40-42).

Kupitia nukuu hii, msomaji anapata picha halisi ya maisha ya shuleni. Ni kweli wapo wanafunzi wanaoenda kinyume na sheria za shule. Wakibainika, hatima zao huwa ni kufukuzwa shule. Kwa hiyo, kwa kutumia mhusika Rosa, msanii analeta uhalisia wa kile kilichoandikwa huku akiakisi maisha halisi ya binadamu.

Halikadhalika, kuimarisha uhalisia wa riwaya, msanii anaonesha tukio la kifo. Kifo kinaweza kueleweka kama kipengele kinachofanya matukio ya riwaya yaangazie maisha halisi. Hii ni kwa sababu kifo ni sehemu ya kawaida na isiyoweza kuepukika katika maisha ya binadamu. Mwandishi anapomwonesha mhusika akikabiliwa na kifo au hatimaye kufariki, anaiweka riwaya katika mazingira yanayofanana na maisha ya jamii. Maisha ambayo yamejawa na misukosuko huku watu wakishuhudia vifo vya ndugu, marafiki au watu wanaowazunguka.

Hivyo, katika *Rosa Mistika*, kifo cha Rosa kinaweza kutumika katika hoja hii kwa sababu kinaonesha kwamba maisha ya mhusika hayamaliziki kwa namna ya kubuniwa na isiyowezekana. Bali maisha yanaweza kufanana na hatima inayoweza kumpata mtu katika maisha halisi. Kifo chake kinakuwa sehemu ya mfululizo wa changamoto na migogoro aliyopitia. Kwa hali hiyo, migogoro hiyo humfanya msomaji kulitazama tukio hilo kama jambo linalowezekana katika uhalisia wa jamii. Mwandishi anasema:

Rosa aliona ulimwengu wote ukimuonea huruma, lakini sasa aliona
kanakwamba ulimwengu wote ulikuwa ukimcheka. Kuishi aliona hawezi.
Aliona ni fedheha. Alitafuta chupa ... akaisagasaga juu ya jiwe ... aliweka ule
ungaunga wa vipande vya chupachupa ndani ya glasi. Aliweka maji ... mara
moja alikunywa yale maji ...

Rosa hakujitingisha. Honorata alitambua kwamba Rosa alikuwa hapumui.
Alitambua kwamba Rosa alikuwa amekufa ... (uk. 140-142).

Tukio hili linakaribiana na uhalisia wa maisha ya kila siku, ambapo kupitia wahusika mviringo, mwandishi anakuwa huru kuipa uhai yake kwa kuendana na mazingira halisi ya binadamu. Kwa jumla, uundaji wa wahusika mviringo katika *Rosa Mistika* umechangia kuimarisha uhalisia wa



riwaya kwa kuwahusisha wahusika na matukio na changamoto zinazochukua na maisha halisi ya jamii. Matukio kama migogoro ya kifamilia, mahusiano ya kimapenzi, mateso, na kifo yanapowasilishwa kupitia wahusika wenye hisia, maamuzi, na mwikio changamani, humfanya msomaji kuyaona matukio hayo kama sehemu ya mambo yanayoweza kutokea katika jamii. Hali hii inaafikiana na Nadharia ya Uhalisia, ambayo kwa mujibu wa Wamitila (2002) inasisitiza usawiri wa maisha ya kila siku kwa uyakinifu. Fauka ya hayo, inazidisha msisitizo uliowekwa na Wafula na Njogu (2007) unaobainisha kwamba wahusika wanapaswa kusawiriwa kiyakinifu ili kuakisi maisha halisi ya jamii. Kwa msingi huo, uundaji wa wahusika mviringo haujatumiwa tu kuwafanya wahusika waonekane, bali pia umemwezesha mwandishi kuwasawiri katika mazingira na matukio yanayofanana na yale yanayowakabili binadamu katika maisha halisi, hivyo kuifanya riwaya iwe na uhalisia na ushawishi zaidi kwa msomaji.

Kuibua Migogoro ya Ndani na Nje

Uundaji wa wahusika mviringo ni muhimu katika kuibua migogoro ya ndani na nje katika riwaya. Kwa upande wa migogoro ya ndani/binafsi, mhusika anaweza kukabiliwa na hali ya kusita, hofu, majuto, tamaa au mkanganyiko wa kufanya maamuzi. Jambo hilo, humrahisishia msomaji kuelewa kwa kina hali ya kisaikolojia ya mhusika. Kwa upande mwingine, migogoro ya nje/ mgogoro wa mtu na mtu hujitokeza kupitia mahusiano ya mhusika na familia, wapenzi, marafiki, na jamii kwa jumla. Wahusika wa aina hii, hujengwa kwa kupewa hisia, mawazo, matamano, mitazamo, na misimamo inayoweza kubadilika kulingana na mazingira wanayokutana nayo. Hali hii humwezesha mwandishi kuonesha migongano inayotokea ndani ya nafsi ya mhusika, pamoja na migongano inayojitokeza kati yake na wahusika wengine au mazingira yanayomzunguka. Hivyo, uundaji wa wahusika mviringo huifanya migogoro katika riwaya iwe ya kina na isawiri uhalisia wa kijamii.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mgogoro wa ndani unaonekana kupitia kwa mhusika Rosa. Mgogoro huu, unajitokeza katika kipindi ambacho Rosa anaanza kukabiliana na maisha yake ya kimapenzi na matokeo yanayotokana na mahusiano yake. Hii ni baada ya kutoka katika malezi ya nyumbani yenye udhibiti wa wazazi na kuingia katika mazingira ya shule ya bweni. Rosa anakutana na mazingira mapya yenye uhuru na vishawishi vinavyomweka katika hali ya kufanya maamuzi tofauti na matarajio aliyolelewa nayo. Hali hii inamweka katika mvutano kati ya malezi, maadili, na matarajio ya jamii kwa upande mmoja. Upande mwingine, anavutwa na matamano pamoja na mahusiano anayokutana nayo katika maisha yake. Katika ukurasa 46 mwandishi anaonesha jinsi Rosa anavyojuliza kipi kitamkuta kama akiamua kuwa na mahusiano na wanaume. Mwandishi anasema:

Rosa alianza kufikiri kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yuko Ukerewe mimi nipo Usukumani. Baba anakaa akinichunga, anafikiri yeye atania? (Uk. 46).

Katika nukuu hii, mwandishi anaonesha jinsi Rosa anavyojishauri ili kubadili mwenendo wa maisha yake huku akijiandaa kukabiliana na matokeo ya maamuzi yake. Mgogoro huu, unaisha pale Rosa anapoamua kuingia kwenye mahusiano na Deogratius. Hivyo basi, utokeaji wa Rosa kama mhusika mviringo unamwezesha mwandishi kuonesha kwa kina mvutano wa kisaikolojia unaoweza kumpata binadamu anapokabiliana na matamano yake, malezi, na matarajio ya jamii. Kwa hali hiyo, mgogoro wa ndani wa Rosa unaongeza kina cha mhusika na kumfanya aonekane kama mhusika mwenye fikra, hisia, na maamuzi yanayobadilika kulingana na mazingira anayopitia.

Vilevile, mgogoro wa nje katika *Rosa Mistika* unaonekana kupitia mvutano unaojitokeza kati ya Rosa na wahusika wenzake pamoja na mazingira yanayomzunguka. Kwa mfano, Rosa anakabiliwa na



mgogoro na baba yake. Bwana Zakaria, anatumia ukali, vitisho, na vipigo kumdhibiti na kumlazimisha Rosa kufuata misingi ya malezi aliyomwekea. Mgogoro huu, unafikia hatua ambapo Rosa anampinga baba yake waziwazi na kumwambia kwamba tangu wakati huo yeye si baba yake, naye si mtoto wake. Maelezo haya yanaonekana pale Rosa anapoongea na baba yake:

Kila wakati unatuchunga. Unafikiri utatua wewe? ... Rosa tangu leo wewe si mtoto wangu. Tangu leo wewe si baba yangu. Rosa alidakia bila kukawia ... Stella alimweleza Rosa jinsi Zakaria alivyonoa panga kumkata vipandevipande kama angalirudi nyumbani siku ile (uk. 85 -87).

Nukuu hii, inaonesha mgogoro kati ya Rosa na baba yake. Mbali na Rosa kumjibu baba yake kwa ukali, mwandishi anaonesha kuwa Rosa aliondoka nyumbani na hakurudi.

Halikadhalika, Rosa anaingia katika migogoro na wanaume anaohusiana nao. Hili linatokea pindi mahusiano hayo yanapokinzana na matarajio yake au/na yanapomweka katika mazingira magumu. Tunamwona Rosa akigombana na mke wa Mwalimu Thomas. Mgogoro huu, unasababisha Rosa kujeruhiwa huku wanafunzi wenzake wakianza kumchukia na kumtemea mate. Mwandishi anasema:

Mle ndani wote wawili walishangaa kusikia mlango ukigongwa kwa ghadhabu. Mwalimu mkuu wa chuo alitambua kwamba huyo alikuwa ni mke wake ... Rosa pombe ilimtoka alianza kukimbia huku na huko ... Mlango ulipasuka ... Mke wa mwalimu aliingia na shoka lake mkononi ... Rosa aliangukwa chini, yule mwanamke alimuinamia. Rosa alitiwa jino. Palepale uso wa Rosa ulienea damu. Yule mwanamke alionekana akitema kitu fulani chini (uk. 78).

Nukuu hii, inaonesha jinsi Rosa alivyofumaniwa na mke wa Mwalimu. Hitimisho la mgogoro huu ni Rosa kuwa kilema wa sikio maisha yake yote. Pia, katika ukurasa wa 140, Rosa anakabiliwa na mgogoro na Charles. Hii ni baada ya Charles kukataa kumwoa kutokana na historia yake isiyofaa ya mahusiano ya kimapenzi. Kukataliwa huko kunasababisha Rosa kuwa na mgogoro binafsi uliochangia katika uamuzi wake wa kujiua.

Kimsingi, uundaji wa wahusika mviringo katika *Rosa Mistika* umechangia kwa kiasi kikubwa, kuibua migogoro ya ndani na nje inayosukuma maendeleo ya riwaya. Uwezo wa wahusika hawa kuwa na hisia, mitazamo, na maamuzi yanayobadilika umemwezesha mwandishi kuonesha kwa kina mivutano inayotokea ndani ya nafsi za wahusika. Hali hii inaafikiana na Nurgiyantoro (2013), anayebainisha kuwa mgogoro wa ndani hutokea katika nafsi ya mhusika, ilhali mgogoro wa nje hutokana na upinzani kati ya mhusika na kitu kilicho nje yake, yakiwamo mazingira ya kibinadamu. Kwa upande mwingine, Wafula na Njogu (2007) wanaonesha umuhimu wa kuvitazama vipengele vya kifasihi kama sehemu zinazohusiana katika kujenga kazi nzima ya fasihi. Kwa msingi huo, migogoro inayowakabili wahusika katika *Rosa Mistika*, haijajitokeza kwa ajili ya kuendeleza matukio pekee bali, pia, kufanya ukamilifu wa simulizi husika. Kimantiki, uviringo umekuwa ni nyenzo muhimu ya kufichua hali za kisaikolojia, mahusiano, na misimamo ya wahusika. Hivyo, uundaji wa wahusika mviringo umeifanya migogoro iwe na kina na kuifanya riwaya iwe na mvuto na uhalisia zaidi kwa msomaji.

Husaidia Kuendeleza Maudhui

Uundaji wa wahusika mviringo ni muhimu katika kuendeleza maudhui kwa sababu mabadiliko yao ya kitabia, kimawazo, na kihisia huwezesha dhamira na masuala mbalimbali ya kijamii kujitokeza na kuendelea kutoka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Wahusika wanapokabiliana na



mazingira na matukio mbalimbali, hufanya maamuzi na kuchukua hatua zinazoendeleza maudhui yanayolengwa na mwandishi. Hivyo, maudhui hayabaki katika kiwango cha kutajwa tu, bali hujengwa na kuendelezwa kupitia matendo, mahusiano, migogoro, na mabadiliko ya wahusika.

Katika *Rosa Mistika*, hali hii inaonekana kupitia maisha ya Rosa, ambaye matendo na maamuzi yake katika maisha ya kimapenzi yanakuwa chanzo cha mfululizo wa matukio yanayoendelea kujenga maudhui ya riwaya. Kujihusisha kwake katika mahusiano ya kimapenzi kunahusishwa na kuporomoka kwa masomo yake, kusimamishwa au kufukuzwa shule, na baadaye kukabiliwa na changamoto nyingine katika maisha yake. Aidha, mahusiano yake ya baadaye na Thomas yanamwingiza katika mgogoro na mke wa Thomas hali inayosababisha kupigwa na kujeruhiwa. Mfululizo huu, unaonesha kwamba tukio moja linalohusishwa na maamuzi ya mhusika linaweza kusababisha tukio jingine na, hivyo, kusukuma mbele matukio na kuendeleza maudhui ya riwaya. Kwa mantiki hiyo, uundaji wa uviringo wa Rosa unamwezesha mwandishi kuendeleza maudhui kupitia mnyororo wa matendo, maamuzi, na matokeo anayopitia katika maisha yake. Kwa mfano, katika ukurasa wa 50 mwandishi anaonesha Rosa akifukuzwa shule. Hii ni baada ya kubainikika kuwa na mahusiano na wanaume mbalimbali hali inayomfanya ashuke kimasomo. Mwandishi anasema:

Masista walishangaa kumwona Rosa anateremka sana katika mitihani yake.
Lakini Sista John alikuwa ameshavumbua. Alikuwa ameshasikia kuhusu
tabia na matendo yake nje ... Rosa tumekusudia kukupeleka nyumbani.
Utarudi tu kufanya mtihani wako wa Cambridge. Rosa alilia (uk. 50).

Nukuu hii, inaonesha jinsi tukio moja linavyosababisha kutokea kwa matukio mengi, ambayo yanapelekea kusonga mbele kwa riwaya. Tukio la Rosa kujihusisha na wanaume wengi, ndicho chanzo cha kutokea kwa matukio mengi ambayo mwandishi ameyafafanua katika riwaya hii.

Kwa upande wa mhusika Flora, naye kutokana na uviringo wake matukio yake, yanachangia katika kuipeleka mbele simulizi ya hadithi. Flora anaoneshwa akiishi pamoja na mchumba wake katika mazingira ambayo jamii inayazungumzia kwa mtazamo hasi. Hali hiyo inaenda sambamba na kushuka kwa maendeleo yake ya kielimu, ambapo matokeo ya mtihani yanaonesha kuwa amefeli na hata hakufaulu kupata GCE. Mwandishi anasema:

... huko ndiko Flora alikokuwa akiishi pamoja na mchumba wake. Watu
wengi walisema kwamba Flora alikuwa akiishi kama kimada. Flora
hakuonesha dalili yoyote ya kupata mimba. Majibu yake ya mtihani wa
Cambridge yalipokuja Flora alikuwa palepale nyumbani. Majibu
hayakumstusha hata kidogo. Flora alishindwa, hata GCE hakupata (uk. 130).

Kimsingi, dondoo hilo linadhihirisha kwamba tabia ya Flora ya kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi inahusishwa na kuporomoka kwa maendeleo yake ya kielimu. Kitendo hicho kinazalisha tukio jingine linaloendeleza masimulizi. Mhusika Flora, kwa namna hiyo, anakuwa sehemu muhimu ya kuendeleza maudhui yanayohusu athari za mahusiano ya kimapenzi kwa maisha na elimu ya vijana. Hii ni kwa sababu matendo yake yanazaa matokeo yanayoendeleza matukio ya riwaya. Hivyo, uundwaji wake kama mhusika mviringo unamwezesha mwandishi kuendeleza maudhui kupitia mabadiliko ya maisha, maamuzi, na matokeo anayoyapata.

Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba wahusika mviringo si wahusika wa kubeba matukio pekee, bali matendo na maamuzi yao ndiyo yanayosaidia kuzalisha na kuendeleza matukio yanayobeba maudhui ya riwaya. Hili linaungwa mkono na Mbijima (2025) anayebainisha kuwa ujitokezaji wa vipengele vya fani na maudhui hutegemea kwa kiasi kikubwa namna mwandishi anavyowaumba



wahusika. Aidha, Nurgiyantoro (2018) anaeleza kuwa matukio na migogoro ni vipengele muhimu katika maendeleo ya ploti, huku migogoro ikichangia kuendeleza ploti ya kazi ya kifasihi. Kwa hiyo, uundaji wa wahusika mviringo katika *Rosa Mistika* umewezeshwa maudhui kujengwa na kuendelezwa hatua kwa hatua kupitia matendo, maamuzi, na matokeo yanayowakabili wahusika.

Kuongeza Mvuto wa Kisanaa wa Riwaya

Uundwaji wa wahusika mviringo huongeza mvuto wa kisanaa wa riwaya kwa kuifanya kazi ya fasihi, ivutie na kumfanya msomaji awe na hamu ya kuendelea kufuatilia visa na matukio yanayowahusu wahusika hao. Mvuto wa kisanaa katika riwaya hujitokeza kupitia msuko mzuri wa visa na matukio, uundaji wa wahusika wenye kuvutia, pamoja na matumizi ya mitindo mbalimbali ya kisanaa, hususani lugha inayomvutia msomaji. Wahusika mviringo huchangia vipengele hivi kwa sababu mabadiliko yao ya kitabia, kimtazamo, na kihisia huibua matukio na migogoro mbalimbali, ambayo huendeleza msuko wa riwaya. Aidha, uchangamano wa wahusika hufanya matukio yasiwe ya kutabirika kwa urahisi, hali ambayo huongeza udadisi wa msomaji.

Katika *Rosa Mistika*, mwandishi anatumia lugha inayomvutia msomaji ili kumjenga mhusika kwa maelezo ya kina. Mwandishi anaelezea mwonekano wa Rosa wa unyenyekevu, unyamavu na hata mwenendo wake wa kila siku. Hivyo, inathibitisha uundaji wa mhusika kwa ustadi ambao ni sehemu ya mvuto wa kisanaa. Katika kudhihirisha hili mwandishi anasema:

Rosa alikuwa msichana mzuri, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mnyamavu. Kama akienda kuoga kisimani utamwona kabla ya kuvua nguo anaanza kuangalia huku na huko, huvua, huoga upesiupesi, huvaa, huchukua maji na kurudi nyumbani. Alikuwa hapendi kuangaliwa kwa muda mrefu. Ukimwangua machoni huinamisha kichwa (uk. 3).

Katika nukuu hii, mwandishi anatumia lugha ya mvuto ili kumjenga mhusika mviringo. Jambo hili linaibua taswira kwa msomaji na kunogesha mvuto wa riwaya. Halikadhalika, msuko mzuri wa visa na matukio huongeza mvuto wa kisanaa katika riwaya. Mabadiliko ya kitabia, kimtazamo, na kihisia ya wahusika huibua migogoro na matukio mbalimbali yanayosaidia kuendeleza simulizi. Katika *Rosa Mistika*, mabadiliko aliyopitia Rosa yanasababisha kutokea kwa matukio na migogoro mbalimbali. Jambo linalomfanya msomaji kuwa na hamu ya kufuatilia kinachofuata. Mwandishi ameweka mfululizo wa matukio ya Rosa kutoka katika malezi ya nyumbani, kupelekwa shule ya bweni, na kukutana na mazingira mapya. Mengine ni kuingia katika mahusiano, kupata matatizo, pamoja na kuachwa na Charles hadi kufikia uamuzi wa kujiua. Kwa mfano, kuvunjika kwa uhusiano wake na Charles, kunatokana na historia ya mahusiano yake ya kimapenzi. Tukio hili linasababisha kifo cha Rosa. Mwandishi amelionesha hili katika ukurasa wa 144 - 146. Kimsingi, mantiki ya msuko huu wa matukio ni kumfanya msomaji kutaka kufahamu hatua inayofuata na hatima ya mhusika. Hali hiyo, inaongeza mvuto wa riwaya.

Kwa ujumla, uundwaji wa wahusika mviringo kumeongeza mvuto wa kisanaa katika *Rosa Mistika* kwa kuwafanya wahusika waonekane wa kweli, wenye hisia, mitazamo, na mabadiliko yanayoweza kujitokeza katika maisha halisi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uhalisia, wahusika wanapaswa kusawiriwa kiyakinifu ili kuakisi maisha ya kila siku ya jamii, huku matukio yakioneshwa kwa namna inayokubalika katika uhalisi wa maisha (Kasiga, 2022). Kwa msingi huo, mabadiliko ya mitanziko inayowakabili wahusika katika *Rosa Mistika* huifanya riwaya iwe na uhai na kumfanya msomaji kujihusisha na hatima ya wahusika. Hoja hii imethibitishwa na Fuluge (2024) anayebainisha kuwa mitanziko ya wahusika katika *Rosa Mistika* inasawiri wahusika halisi wanaokumbana na changamoto katika maisha ya kila siku. Hivyo, wahusika mviringo huunganisha



usanii na uhalisia wa maisha kwa shabaha ya kuifanya riwaya kuwa yenye mvuto zaidi kwa wasomaji.

Hitimisho

Uundwaji wa wahusika mviringo ni kipengele muhimu katika ujenzi wa riwaya kwa sababu humwezesha mwandishi kuwasawiri wahusika kama viumbe wenye maisha na uzoefu unaobadilika. Kupitia wahusika wa aina hii, msomaji huweza kufuatilia kwa karibu safari ya maisha ya mhusika, kuelewa sababu za mabadiliko yake, na kuhusisha matukio ya kifasihi na hali zinazoweza kujitokeza katika maisha ya binadamu. Uchambuzi wa *Rosa Mistika* umeonesha kuwa wahusika mviringo wana nafasi kubwa katika kuipa riwaya uhai na kuifanya iwe na maana kwa msomaji. Kwa hiyo, uundwaji wa wahusika mviringo unapaswa kupewa uzito katika uandishi na uchambuzi wa riwaya za Kiswahili kwa kuwa ni sehemu muhimu ya kuifanya kazi ya kifasihi iwe ya kina na ya mvuto. Kwa kuzingatia umuhimu huo, makala hii inapendekeza kuendelea kuwajenga wahusika kwa namna inayowapa nafasi ya kukua na kubadilika kutokana na mazingira wanayopitia. Vilevile, tafiti zifanyike kuhusu wahusika mviringo katika riwaya, tamthiliya, na filamu za miaka ya hivi karibuni ili kuongeza uelewa kuhusu nafasi yao katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

Marejeleo

- Fishelov, D. (1990). Types of character, characteristics of types. *Style*, 24(3), 422 – 439.
- Fuluge, A. (2024). Mitanziko ya wahusika katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi. *Kioo cha Lugha*, 22(1), 90 – 111.
- Gouldin, G. (1961). *Realism, heroines, Flaubert* (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa). University of Richmond.
- Kasiga, G. A. (2022). *Tathimini ya U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania* (Tasnifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. East African Literature Bureau.
- Lucey, M. (2011). *Realism*. Katika W. Burgwinkle, N. Hammond na E. Wilson (Wah.), *The Cambridge history of French literature*, 461– 470. Cambridge University Press.
- Lukács, G. (1999). *Balzac et le réalisme français*. La Découverte.
- Lyatuu, J. (2011). *Usawiri wa wanawake katika fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa waandishi wa kike na wa kiume – uchunguzi katika riwaya teule* (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Makame, M. I. (2018). *Usawiri wa wahusika vijalunga katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Rosa Mistika na Watoto wa Mama N'tilie* (Tasnifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1995). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam University Press.
- Mbijima, R. J. (2025). Wahusika wa kivisasili na athari yake katika riwaya ya Kiswahili. *Mulika*, 44(2), 248 – 267.
- Msigala, S. H. (2024). Mkengeuko wa malezi kwa wahusika katika riwaya ya *Rosa Mistika*. *Kioo cha Lugha*, 22(1), 149 – 163.
- Muia, S. T., Mutua, J., na Makoti, V. (2023). Usawirishaji wa uhusika katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*. *Research Journal in African Languages*, 4(2).
- Njogu, K. na Chimera, R. M. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Nkinde, M. (2011). *Motifu za safari na msako katika makuzi ya wahusika wa riwaya za E. Kezilahabi* (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Nurgiyantoro, B. (2018). *Teori pengkajian fiksi*. UGM Press.
- Nyandwaro, L. K. (2024). *Usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya Harusi ya Wendawazimu*.



East African Journal of Swahili Studies, 7(2), 46 – 59.

Ponera, A. S. na Kasiga, G. A. (2019). Mdhihiriko wa kionjo cha usangwini kwa mhusika Willy Gamba katika riwaya ya *Njama*. *Kioo cha Lugha*, 17, 99 – 113.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2024). Miangwi ya kimtindo, kidhamira na uhusika: Uchunguzi wa kazi teule. *Kioo cha Lugha*, 22(2), 182 – 195.